

**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE  
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA MAHAFALI YA  
KIDATO CHA NNE 2023 SHULE YA SEKONDARI MSAKILA  
TAREHE 16 SEPTEMBA, 2023**

- ***Mhasham Beatus Urassa, Askofu wa Jimbo Katoliki la Sumbawanga***
- ***Afisa Elimu Mkoa,***
- ***Sr. Pudensiana Tarimo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Msakila***
- ***Wajumbe wa Bodi ya Shule,***
- ***Waalimu,***
- ***Wanafunzi,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema ambaye ametuwezesha kuwa hapa leo tukiwa na afya njema. Kipekee niwashukuru sana Wanajumuiya wote wa Shule ya Sekondari Msakila kwa kunialika kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya Kidato cha NNe, 2023. Kipekee nimpongeze sana Mhasham Beatus Urassa Askofu wa Jimbo Katoliki la Sumbawanga kwa juhudini kubwa anazoendelea kuzifanya katika Jimbo lake la Sumbawanga katika Nyanja mbalimbali na hasa Elimu na Afya.

Aidha, ninampongeza tena Mhashamu Baba Askofu Beatus Urassa ALCP/OSS na Waandamizi wake kwa jitihada zake za kujenga shule nzuri

yenye viwango na inayokidhi mahitaji ya Elimu na kuifanya Msakila Sekondari kuwa sehemu sahihi kwa ajili ya malezi bora na Elimu bora.

**Ndugu Washiriki**, Serikali yetu ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa ikisisitiza kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na huu uliofanywa na Kanisa Katoliki Jimbo la Sumbawanga la ujenzi wa Shule hii nzuri. Serikali pia imeendelea kuhakikisha kuwa tunakuwa na sera nzuri za Elimu zitakazowasaidia walimu na wanafunzi kuinua ufaulu.

**Ndugu Washiriki**, nitumie fursa hii kuwakumbusha wanafunzi wote kusoma kwa bidi na maarifa ili kuleta matokeo yanayoendana na mazingira mazuri ya shule hii yaliyowekwa na Mhasham Baba Askofu Beatus Urassa. Aidha, niwakumbushe wanafunzi wote kuendelea kudumisha nidhamu na ushirikiano na walimu wenu ili kuleta matokeo chanya. Upo msemo kuwa Mwanafunzi mwenye nidhamu hupata matokeo mazuri kuliko yule ambaye hana nidhamu.

**Ndugu Washiriki**, wazazi wote niwakumbushe wajibu wenu wa kuhakikisha kuwa mnawalea watoto wenu katika maadili yampendezayo Mwenyezi Mungu ili kuleta matokeo chanya. Aidha, ni jukumu lenu wazazi kumuunga mkono Mhasham Baba Askofu kwa kuhakikisha kuwa mnatoa ada kwa wakati na kwa namna mlivyopangiwa na shule kwani kufanya hivyo kunaongeza ufanisi wa Msakila Sekondari na kumpa urahisi Mkuu wa Shule wa uendeshaji wa shule hii. Aidha, niwaombe wazazi wenyewe uwezo wawapeleke watoto wao Msakila Sekondari kumuunga mkono baba Askofu kwa kuwaleta kusoma kwenye Shule hii.

**Mwisho**, niwaombe wote mlionhudhuria Mahafali ya Vijana wetu hawa wa Kidato cha Nne hapa Msakila Sekondari mwaka huu 2023 tuendelee kuwaombea ili Mungu awabariki watoto wetu na kuwapa matokeo mazuri.

Mungu Ibariki Tanzania

Mungu bariki Mkoa wa Rukwa

Mungu bariki Msakila Sekondari

Asanteni kwa kunisikiliza

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**